**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI- MAFINGA**

Mafinga Town Council

**Kumb. Na: HM/MAF/A.60/28/III/90** **Tarehe: 20/05/2025**

# TANGAZO LA FURSA ZA MIKOPO YA ASILIMIA 10

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mafinga anapenda kuwajulisha wananchi wote walioomba mikopo baada ya mikopo kurejeshwa kwamba Halmashauri inatarajia kuanza mchakato wa utoaji wa mikopo kwa vikundi ambavyo havikufanikiwa kupata mikopo awamu iliyopita. Ikumbukwe kuwa vikundi hivi tayari vilishasajiliwa na kuomba mikopo kupitia mfumo.

Aidha kwa kata ya **BUMILAYINGA** na **SAOHILL** mchakato unaanza upya kwakuwa hakuna vikundi ambavyo vilivyosalia ambavyo havikupata mkopo awamu iliyopita. Fedha zilizopo kwa ajili ya kukopeshwa ni shilingi **428,795,879/=**

**Vikundi vitakavyoomba mikopo vinatakiwa kuwa na sifa zifuatazo;**

i. Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri.
ii. Kikundi kiwe kinajishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati.
iii. Kikundi cha wanawake na kikundi cha vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano **(5)** na kuendelea.
iv. Kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wananakikundi wasiopungua wawili. Aidha kwa kuzingatia kanuni ya **6a(1)** mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zinafanana na sifa za vikundi vingine.
v. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na
vi. Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka **18** na kuendelea. Aidha kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka **18** hadi **45**

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Afisa Maendeleo wa kata yako

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **27/05/2025**

**Tangazo hili limetolewa na;**

*Dorothy Kobelo*
**KAIMU MKURUGENZI WA MJI**
**HALMASHAURI YA MJI**
**MAFINGA**

MKURUGENZI HALMASHAURI YA MJI - MAFINGA
S. L. P. 76
MAFINGA